**TAMKO LA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU KUHUSU HALI YA HAKI ZA BINADAMU KATIKA TARAFA YA NGORONGORO**

**1.0 Utangulizi**

Sisi asasi za kiraia na watetezi wa haki za binadamu Tanzania, tunatoa taarifa hii kueleza hali ya haki za binadamu kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro wilaya ya Ngorongoro mkoa wa Arusha kama ifuatavyo. Tumeguswa na hali ya sasa inayoendelea katika tarafa ya Ngorongoro ambapo wananchi takribani 40 elfu wapo katika mgomo na maandamo ya amani siku ya tano sasa bila kusikilizwa na viongozi wa juu wa nchi. Tunatoa tamko hili kuonyesha masikitiko yetu na kuishauri serikali hasa Mhe Rais Samia Suluh Hassani aone umuhimu wa kuwasikiliza watu hawa kwa kuwa wanaendelea kuumia kwa njaa na baridi kando kando ya Barabara ambapo wapo siku ya tano sasa.

Wilaya ya Ngorongoro ina jumla ya Tarafa tatu ambazo ni Tarafa ya Sale , Tarafa ya Ngorongoro na Tarafa ya Loliondo. Jumla ya ukubwa wa eneo la wilaya ya Ngorongoro ni Kilmeta za Mraba 14,000 elfu ambayo Tarafa ya Ngorongoro pekee inachukua asilimia 55 ya eneo lote hili. Kwa mujibu wa Sensa ya 2022 Wakazi wa Wilaya Ngorongoro kwa ujumla ni watu 270,000 na Tarafa ya Ngorongoro Pekee ina takriban nusu ya jumla ya wakazi wa Wilaya ya Ngorongoro. Tarafa ya Ngorongoro ina kata 11 kati ya kata 28 za Wilaya Ngorongoro na Vijiji 25 sawa na nusu ya vijiji vyote vya Wilaya Ngorongoro. Toka zoezi hili la watu kuhamishiwa Msomera kuanza takwimu zetu zinaonyesha watu waliokwisha hamia Msomera ni 9600 ( sawa na asilimia 8) na waliobaki kwa sasa Ngorongoro ni 110,000. Watu hawa laki moja na elfu kumi ndio wanapitia hizi changamoto za sasa katika Tarafa ya Ngorongoro. Pia kumekuwa na udanganyifu na propaganda inayofanyika na wanaosimamia zoezi hili kwa kuonyesha kuwa watu wameisha katika Tarafa ya Ngorongoro. Kati ya hawa watu laki moja wanaoshiriki maandamano ni vijana wa rika zote waume kwa wake ambao ni takriban 40 elfu wakati waliobaki majumbani ni watoto, wanawake wajawazito, wagonjwa na wazee wa umri mkubwa.

**2.0 Changamoto kubwa kwa sasa katika Tarafa ya Ngorongoro**

**a) Usitishwaji Wa Huduma Muhimu Za Kijamii Na Vikwazo Vya Maendeleo**

Baada ya sisi watetezi wa haki za binadamu kufanya ziara ya ufuatiliaji Ngorongoro na Handeni mwaka 2023 , tulibaini kuwa mwaka 2022 huduma za jamii (Elimu, Afya, Maendeleo n.k) zilisitishwa ama kuzoroteshwa katika tarafa ya Ngorongoro. Taarifa hii ya Watetezi wa Haki za Binadamu inaonyesha kuwa huduma hizi zimezoroteshwa kwa kuzuia ujengaji wa shule mpya, madarasa mapya, zahanati na vituo vya afya vipya, pia visima vya maji na matundu ya vyoo. Pia ukarabati wa majengo ya huduma hizi za msingi kwa jamii zilisitishwa. Njia nyingine iliyotumika ni kuhamisha fedha za miradi ya maendeleo kutoka TAMISEMI kama vile miradi ya Burst na miradi kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Kwa mfano mwaka 2022 jumla ya shilingi 195,500,000 zilihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga. Kiasi cha shilingi za kitanzania 355,500,000 za mradi wa uviko-19 (Covid-19 relief funds) zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika tarafa ya Ngorongoro zilihamishiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni bila kuazimiwa na

baraza la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya kujenga madarasa na mabweni ya wanafunzi katika shule tatu za Serikali ambazo ni Nainokanoka, Embarway na shule ya Wasichana ya Ngorongoro pamoja na shule za msingi Endulen, Misigiyo na Esere. Fedha zote za Tarafa ya Ngorongoro kwa sasa haziendi tena katika taarafa hii.

Mnamo 08/04/2022 Serikali ilisitisha huduma ya afya ya dharura iliyokuwa inatolewa na Flying Medical Service. Flying Medical Service ilikuwa inatoa huduma mbalimbali za afya kama vile huduma ya chanjo kwa watoto, huduma ya kliniki kwa wajawazito, wagonjwa wa kifua kikuu, na magonjwa ya dharura. Huduma hiyo ilikuwa inatolewa hasa katika maeneo ambayo hayafikiki kwa usafiri wa kawaida. Kati ya mwaka 1985 hadi mwaka 2021 Flying Medical Service iliwafikia jumla ya wagonjwa 765,947 ambapo watoto pekee ni 138, 036.
Wananchi hawa wamekuwa katika mazingira magumu sasa na kuishi kama watu waliotengwa katika nchi yao. Wapo katika mazingira magumu sana yanayokiuka haki zao za msingi kama binadamu na pia kama raia wa Tanzania na ikiwa na matokeo hasi na ya moja kwa moja kwa jamii hii ya Wamaasai ikiwa ni pamoja ya yafuatayo.

i) Kuathiri Kizazi cha sasa na Kizazi kijacho cha jamii ya Wamaasai kuhusu uendelevu wao wa kielimu.
ii) Kuongeza hali ya utegemezi uliopitiza kwa jamii hiyo hali inayopelea kutweza utu wao na kuongezeka kwa vitendo vya uminywaji haki kwa makundi maalum, hasa wanawake, watoto, wazee, na watu wenye ulemavu.
iii) Kuhatarisha Maisha ya jamii ya Kimaasai kwa kukosa huduma za afya hususani kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ambao kinga zao bado hazijaimarika, wazee pamoja na wanawake.
iv) Kuhatarisha ustawi wa vijana wa jamii hiyo na kuchochea kukosekana kwa ustahimilivu wa vishawishi rika kwa vigezo vya kiuchumi hali inayoweza kupelekea kuongezeka kwa mimba za utotoni, Magonjwa na kusitishwa kwa ndoto zao.( SRHR Vulnerabilities).
v) Kuweka jamii ya Kimaasai katika hatari ya kutoweka kabisa kutokana na kutokuwana muelekeo wowote wa kimaisha
vi) Kuongezeka kwa umaskini kwa jamii ya Kimaasai
vii) Tishio la milipuko ya magonjwa na njaa itakayoweza sabababisha maelfu ya watu kupoteza maisha

## b) Kufutwa Kwa Vitongoji, Vijiji Na Kata Zote Katika Tarafa Ya Ngorongoro

Mnamo Juni 26, 2024 Waziri wa TAMISEMI, Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa alisaini Amri ya Marekebisho ya Amri ya Mgawanyo wa Maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya Mwaka 2024 ambayo ilitangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 673 la Agosti 02,2024. Amri hiyo ya marekebisho imefuta kata, vijiji na vitongoji vyote vilivyopo katika tarafa ya Ngorongoro Wilayani Ngorongoro. Tangazo hilo limefuta kata 11, vijiji 25 na vitongoji 96 vyenye idadi ya watu zaidi ya laki moja na elfu kumi (110,000) kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2022.

Tangazo hilo limekiuka haki za msingi za binadamu pamoja na Ibara zifuatazo za katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania:

(i) Ibara ya 13 inayotoa haki ya usawa mbele ya sheria na kupiga marufuku aina yeyote ya ubaguzi kwa mtu au kikundi chochote.
(ii) Ibara ya 14, inayotoa haki ya kuishi, kwasababu watu zaidi ya laki moja na elfu kumi (110,000) wamefutiwa maeneo yao ya kuishi katika tarafa ya Ngorongoro
(iii) Ibara ya 21 (1) na (2) inatoa haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye binafsi au Taifa. Hii ni kwasababu hapakuwa na ushirikishwaji wa aina yoyote kwa wakazi wa tarafa ya Ngorongoro.
(iv) Ibara ya 5 inayotoa haki ya kupiga kura.
(v) Ibara ya 145 na 146 zinazo anzisha serikali za mitaa na kupeleka madaraka kwa wananchi.
(vi) Tangazo hilo pia limekiuka Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ya Mwaka 1959 ambayo malengo yake makubwa ni matatu ambayo ni[1];
    a) Kuendeleza Jamii ya Kifugaji katika tarafa ya Ngorongoro
    b) Kusimamia shughuli za kiuhifadhi ya wanayamapori na mimea
    c) Kusimamia na kuendeleza shughuli za kitalii

Jamii ya Kimaasai kutokana na utamaduni wao na historia yao ya kuishi na Wanyama bila kuwana madhara makubwa, walionekana wanafaa kuendelea kushi katika eneo hili kwa kuwahawana madhara yoyote kwa shuguli za huifadhi. Hivyo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoroilipewa jukumu la kisheria la kuendeleza jamii hii sambamba na shughuli zingine za utalii nauhifadhi[2] ambapo wa Amri ya Waziri inakiuka matakwa haya ya Sheria.

Amri hiyo iliyotolewa na Waziri, imeandikwa kuwa imetolewa chini ya kifungu cha 30 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287. Kifungu hicho hakimpi mamlaka Waziri wa TAMISEMI kufuta vijiji kwa namna yeyote.

Kihistoria wananchi hao wameishi katika maeneo hayo kwa miaka mingi iliyopita hata kabla ya ujio wa wakoloni hadi sasa. Baadhi ya wananchi hao walihamishwa kutoka Serengeti kupisha uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na kuahidiwa kutohamishwa au kubugudhiwa tena kwenye makazi yao katika tarafa ya Ngorongoro. Vilevile Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete alitoa kauli ya Serikali Novemba 23, 2014 kwamba, Serikali haina na haitakuwa na mpango wa kuwahamisha wamaasai wanaoishi Ngorongoro.

[1] Kifungu cha 4 na 6 cha Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro Sura ya 284.

[2]

Kitendo cha kufuta Tarafa nzima yenye nusu ya idadi ya wakazi wa Wilaya nzima ya Ngorongoro ni kosa kubwa sio tu la kikatiba bali ni ukiukwaji mkubwa wa haki na utu wa wananchi wale ambao wamelinda rasilimali hii kwa miaka mingi na hawakustahili kulipwa haya yanawatokea leo.

### c) Kunyimwa Haki ya Kupiga kura Katika Uchaguzi Mwaka 2024/2025

Kabla ya Tangazo hilo la Serikali kutolewa, palikuwepo na malalamiko kuwa wananchi zaidi laki moja ambao ni jamii ya Kimaasai waishio katika tarafa ya Ngorongoro wamenyimwa haki ya kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025 kitendo ambacho kinakiuka haki ya kikatiba ya kupiga kura, kuchaguliwa au kuwachagua viongozi wanaowataka. Uminywaji huu ulijidhirisha katika mambo yafuatayo:

**Mosi**, Tumeona orodha ya vituo vya kupigia kura nchi nzima lakini vijiji vyote vya tarafa ya Ngorongoro havipo. Kwa maana hiyo ni kwamba tarafa ya Ngorongoro hawataweza kupiga kura kwasababu vituo vya kupigia kura vimefutwa katika tarafa nzima.

**Pili**, wananchi wote ambao katika chaguzi zilizopita walijiandikisha kupiga kura katika vituo vilivyopo tarafa ya Ngorongoro kwasasa wanaonekana kwenye mfumo kuwa vituo vyao vya kupigia kura vipo katika kijiji cha Msomera, wilaya ya Handeni mkoa wa Tanga. Tuna idadi kubwa ya watu ambao majina yao wameona majina yao yakiwa katika mfumo wa wilaya ya Handeni. Kwa maana nyingine ni kwamba wananchi wote waliojiandikisha kupiga kura katika tarafa ya Ngorongoro mwaka 2020 sasa wanaonekana watapiga kura katika wilaya ya Handeni wakati wao wapo Ngorongoro. Hii ni kinyume cha Sheria ya Uchaguzi inayomtaka kila mtu kupiga kura katika kituo alichojiandikisha. Tafsiri nyingine ni kwamba wananchi hao zaidi ya laki moja watakuwa wamenyimwa haki yao ya msingi ya kupiga kura au kugombea nafasi za uongozi katika chaguzi zijazo kwa kuwa sio wananchi au wakazi wa Handeni. Hii inadhirisha kuwa zoezi la kuhamisha watu kutoka Ngorongoro sio la hiari kwa kuwa zinatumika nguvu nyingi sana kuweka mazingira magumu wakidhani ndio itapelekea watu kuhama bila kujua kuwa wanakiuka haki za binadamu.

Kuwanyima wananchi zaidi ya laki moja haki yao ya kupiga kura inaweza kuwa na tafsiri zifuatazo:

**i)** Inatia doa kubwa sana kwa Serikali na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuwanyima raia wa Tanzania nusu ya wakazi wa Wilaya ya Ngorongoro ambao zaidi ya laki moja haki ya kupiga kura ikiwemo kuchaguliwa ama kuchagua viongozi wanaowataka.

**ii)** Inaweza pia kutafsiriwa kuwa huu ni ubaguzi unaolenga asili ya mtu au kikundi cha watu au jamii ya wamaasai kwa asili yao. Hii pia ni kunyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania ni mwanachama.

**iii)** Hii pia inaleta wasiwasi juu ya uhuru wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwamba inapokea maelekezo kutoka kwa mamlaka fulani ya juu kuhusu nani apige kura na nani asipige kura, kitu ambacho ni kinyume cha katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**iv)** Inatia doa kubwa katika falsafa ya R nne za Rais Samia alizozitumia vyema kurudisha nchi katika umoja , amani , utulivu na mshikamano.

**3. WITO WETU**

Hatuna tatizo na mkakati wowote ule ambao utakuwa wa hiari na utakaozingatia haki za binadamu katika mchakato wa kutaka kupunguza watu eneo la Ngorongoro. Kama watetezi tulishatembelea maeneo hayo na kutoa mapendekezo yetu ambayo yangezingatiwa tusingekuwa na hizi changamoto leo.

Kusitishwa kwa huduma za kijamii kwa wananchi wakazi wa tarafa ya Ngorongoro kunaleta tafsiri kwamba hilo ni shinikizo la wananchi hao kuhama bila ridhaa yao kutoka kwenye ardhi yao, kuharibu mila na tamaduni zao. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba hata wale ambao wanaweza kwenda maeneo jirani kama Karatu kununua vitu kama bidhaa au mahitaji muhimu ya binadamu wanazuiliwa kuingia na vitu hivyo kwenye geti la kuingia Ngorongoro.

Tunaamani pia kwamba kuwanyima wananchi zaidi ya laki moja haki ya kupiga kura katika tarafa ya Ngorongoro ni njia nyingine ya kuwalazimisha kuhama makazi yao. Nguvu yote hii inayotumika dhidi ya wakazi wa tarafa ya Ngorongoro inadhihirisha kwamba zoezi la uhamisho wa wananchi katika tarafa ya Ngorongoro sio la hiari.

1) Tunamshauri Mhe. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kwenda katika tarafa ya Ngorongoro kuwasikiliza wananchi ili kujua kinaga ubaga changamoto ambazo zinawakabili. Hata katika maandamano ya amani yanayoendelea hivi sasa katika tarafa ya Ngorongoro vilio vya wananchi imekuwa ni kumuomba Mhe. Rais afike Ngorongoro kwaajili ya kuwasikiliza na kutatua kero zao.

2) Tunamsihi Waziri wa TAMISEMI kutengua na kufuta Tangazo la Serikali Na. 673 la 2024 kwani linakiuka katiba, Sheria na Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ambazo Tanzania imesaini na kuridhia.
3) Tunatoa wito kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Kwenda tarafa ya Ngorongoro kwa ajili ya kuandikisha watu ili kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025.
4) Tunaisihi Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kupeleka vituo vya kupigia kura katika tarafa ya Ngorongoro na kuruhusu wananchi kushiriki katika zoezi la kupigia kura.
5) Tunaisihi Tume ya Uchaguzi kuwaondoa kwenye mfumo wananchi wa tarafa ya Ngorongoro ambao taarifa zao zinaonekana zipo katika kijiji cha Msomera, wilaya ya Handeni wakati wananchi hao wapo Ngorongoro. hivyo warejeshwe kwenye mfumo wa awali unaosoma vituo halisi vya Ngorongoro.
6) Tunatoa wito kwa Serikali kuacha kuwabugudhi na kuwabagua wananchi wanaoishi katika tarafa ya Ngorongoro kama zoezi la uhamishwaji ni hiari.
7) Tunasisitiza Serikali ipeleke huduma za kijamii ambazo zimesitishwa kwa miaka mitatu sasa kwenye tarafa ya Ngorongoro ikiwemo huduma za afya.

8) Tunaisihi serikali kusikiliza kilio cha wananchi wa tarafa ya Ngorongoro na kufanyia kazi mahitaji yao. Tunaamini kuwa njia ya mazungumzo ndio njia pekee ya kutafuta suluhisho. Wananchi hawa tumeona katika jumbe zao wakati wa maandamano wapo tayari kwa mazungumzo.
9) Vyombo vya Habari viache kufumbia macho ukiukwaji wa haki za binadamu unaoendelea katika Tarafa ya Ngorongoro.
10) Wadau wa maendeleo hapa nchini wasikae kimya bali waishauri serikali namna bora ya kuendesha zoezi la kuhama kwa hiari bila kuwatesa na kuwabagua wale waliochagua kubaki.

11) Wanaosimamia zoezi la kutaka kuhamisha watu Ngorongoro waache kutumia propanganda za kuwaita watu wa Ngorongoro ni wakenya kwani kufanya hivyo ni kuongeza hasira kwa wnaanchi. Waaache pia kudanganya umma na viongozi wa juu kuwa watu wameisha Ngorongoro.

Taarifa hii imetolewa na asasi za kiraia na watetezi wa haki za binadamu Tanzania leo Agosti 22, 2024 ambazo ni zifuatazo:

| NO. | JINA LA SHIRIKA |
|---|---|
| 1 | Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) |
| 2 | Actions for Democracy and Local Governance (ADLG) |
| 3 | Building Inclusive Society Tanzania Organization (BISTO) |
| 4 | Butemine Gender Awareness and Girls Advocacy (BUGARA) |
| 5 | Christian Education and Development Organization (CEDO) |
| 6 | Civic and Legal Aid Organization (CiLAO) |
| 7 | Shirika la Utafiti wa Kijamii na Huduma za Maendeleo (CORDs) |
| 8 | Crisis Resolving Centre (CRC) |
| 9 | Door of Hope to Women and Youth Tanzania (DHWYT) |
| 10 | Green Leaf Organization (GLO) |
| 11 | Lights for Marginalized Development (LifMADE) |
| 12 | Masafa Early Childhood Foundation |
| 13 | Chama Cha Wafugaji Tanzania |
| 14 | Nishike Mkono Tanzania (NMT) |
| 15 | Rondo Women's Development Organization (ROWODO) |
| 16 | Save the Mother and Children of Central Tanzania (SMCCT) |
| 17 | Sustainable Futures Initiative |
| 18 | TAHECECO |
| 19 | Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC) |
| 20 | Tanzania Tobacco Control Forum (TTCF) |
| 21 | Tanzania Trade and Investment Coalition (TATIC) |
| 22 | The Life Hood of Children and Development (LICHIDE |
| 23 | Tuelimika |
| 24 | Women and Children Welfare Support (WOCWELS) |
| 25 | Kigoma & Ujiji NGOs Network (KIUNGONET) |
| 26 | HakiArdhi |
| 27 | Ujamaa Community Resource Team (UCRT) |

| | |
|---|---|
| 28 | Mtandao wa Mashirika ya Kifugaji (PINGOs Forum) |
| 29 | Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC) |
| 30 | Shirika la Uhifadhi wa Utamaduni wa Kimaasai (Tanzania Maasai Heritage) |
| 31 | Shirika la Kuwabariki Watoto wa Kike na Wanawake wa Jamii za Kifugaji Maasai (NAMGWO) |
| 32 | Shirika la Uhifadhi wa Mifumo ya Asili na Jadi (TEST) |
| 33 | Shirika la Kuinua na Kusaidia Maisha ya Wafugaji (PALISEP) |
| 34 | Shirika la Maendeleo ya Jamii ya Wafugaji wa Kimaasai (MPDO – LARETO) |
| 35 | Tanzania Youth Behavioral Change Organization (TAYOBECO) |
| 36 | Jukwaa la Ardhi Tanzania (TALA) |
| 37 | Shirika la Watu wa Asili na Usimamizi wa Ardhi (FINAL GOVERNANCE) |
| 38 | Green Planet Initiative (GPI) |
| 39 | Mbogwe Legal Aid Organization (MBOLAO) |
| 40 | Ahadi Forum Tanzania (AFTA) |
| 41 | Mulika Afrika |
| 42 | Integrated development initiatives in Ngorongoro (IDINGO) |
| 43 | Jukwaa la Katiba Tanzania |
| 44 | Sauti ya Wanawake Ukerewe |